



Mbuzi, Mbwa na Ng'ombe

- ✎ Fabian Wakholi
- 👤 Marleen Visser, Ingrid Schechter
- 💬 Brigid Simiyu
- 🗣️ Kiswahili
- 📊 Level 2







Mbuzi, Mbwa na Ng'ombe walikuwa marafiki wa karibu sana. Siku moja walisafiri kwa tekisi.




Walipofika mwisho wa safari yao, dereva aliwaomba walipe nauli zao. Ng'ombe alilipa nauli yake.



Mbwa alilipa zaidi kidogo kwa sababu hakuwa na pesa taslimu.




Dereva alipokaribia kumpa Mbwa chenji yake, Mbuzi alitoroka bila kulipa chochote.



Dereva alikasirika sana. Aliondoka bila kumrudishia Mbwa chenji yake.



Hiyo ndiyo sababu hadi leo Mbwa hukimbiza magari ili achungulie ndani kuona kama atampata dereva mwenye chenji yake.



Mbuzi hukimbia anaposikia mlio wa gari. Anaogopa atakamatwa kwa kutolipa nauli.



Na Ng'ombe hababaiki gari likiwa linakuja. Ng'ombe huvuka barabara bila wasiwasi kwa sababu anajua alilipa nauli yake yote.



Storybooks Outline

global-asp.github.io/storybooks-outline

Mbuzi, Mbwa na Ng'ombe

Written by: Fabian Wakholi

Illustrated by: Marleen Visser, Ingrid Schechter

Translated by: Brigid Simiyu

This story originates from the African Storybook (africanstorybook.org) and is brought to you by [Storybooks Outline](https://global-asp.github.io/storybooks-outline) in an effort to provide children's stories in the world's many languages.



This work is licensed under a Creative Commons
[Attribution 3.0 International License](https://creativecommons.org/licenses/by/3.0/).